

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO
(TaSUBa)**



**WITO KWA WASANII KUSHIRIKI KATIKA
TAMASHA LA 41 LA KIMATAIFA LA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO
KUANZIA TAREHE 05 HADI 12 NOVEMBA 2022**

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (zamani *Chuo Cha Sanaa Bagamoyo*) inawakaribisha wasanii na vikundi vya sanaa kwa ujumla kuomba kushiriki kwa kufanya maonyesho katika Tamasha la 41 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo litakalofanyika katika viwanja vya taasisi (TaSUBa - Bagamoyo) kuanzia tarehe **05** hadi **12 Novemba, 2022**.

Tamasha hili limekuwa na malengo mbalimbali ikiwemo kuendeleza na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, kubadilishana uzoefu na kujifunza kutoka kwa wasanii na vikundi vya ndani na nje ya Tanzania kupitia warsha na maonyesho mbalimbali.

Tamasha hili hujumuisha aina mbalimbali za sanaa kama vile *Ngoma, Maigizo, Muziki, Sarakasi, Mazingaombwe, Vichekesho, Filamu* pamoja na maonyesho ya sanaa za ufundi na biashara (**Exhibitions**).

TaSUBa inawakaribisha wasanii na vikundi vya sanaa kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania na nje ya nchi ili kushiriki katika Tamasha hili kongwe la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia;

Barua pepe: bagamoyofest@gmail.com au bagamoyofest@tasuba.ac.tz

Tovuti: www.tasuba.ac.tz

Simu: +255(0) 023 2440032, +255(0) 655 840 405, +255(0) 713 756 168 na
+255(0) 763 408 792